

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI

(Jeshi la Magereza Tanzania)

06 Januari, 2023



TAARIFA KWA UMMA KUHUSU NAFASI ZA AJIRA
ZA KUJIUNGA NA JESHI LA MAGEREZA

Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza anatangaza nafasi za ajira za kujiunga na Jeshi kwa mwaka 2023 kwa vijana wenye elimu ya kidato cha nne (FORM IV).

I. SIFA ZA WAOMBAJI

- a) Awe ni raia wa Tanzania
- b) Awe amemaliza kidato cha nne na kupata ufaulu wa Daraja la I hadi IV
- c) Awe na umri kati ya miaka 18 – 25
- d) Awe na siha njema
- e) Awe amefuzu mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) au aliyepo katika Kambi ya JKT
- f) Asiwe amewahi kuajiriwa Serikalini
- g) Asiwe ameo/kuolewa
- h) Awe tayari kujigharamia katika hatua zote za usaili
- i) Awe na nidhamu na tabia njema na awe hajawahi kupatikana na hatia mahakamani na kuhukumiwa kifungo
- j) Awe na urefu usiopungua futi 5'4 kwa wanawake na futi 5'7 kwa wanaume
- k) Awe tayari kuhudhuria mafunzo ya awali ya uaskari magereza

II. UTARATIBU WA KUTUMA MAOMBI NI KAMA IFUATAVYO :-

Waombaji wote waandike barua kwa Mkuu wa Gereza wa Wilaya husika. Aidha, kwa wilaya zote ambazo hazina gereza maombi yao yatumwe kwa Mkuu wa Gereza lililo jirani. Barua zote za maombi zitumwe kwa njia ya posta. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 05 Februari, 2023.


III. BARUA ZA MAOMBI ZIAMBATISHWE NA NAKALA ZIFUATAZO :-

- a) Nakala ya cheti cha kuzaliwa (Birth Certificate);
- b) Nakala ya cheti cha kuhitimu kidato cha nne;
- c) Nakala ya cheti cha kumaliza shule (Leaving Certificate);
- d) Cheti cha udhibitisho wa siha njema kutoka kwa Mganga wa Serikali;
- e) Nakala ya kitambulisho cha uraia au namba ya utaifa kutoka Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA);
- f) Nakala ya cheti cha kufuzu mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT);
- g) Picha nne (04) za *passport size* ;
- h) Barua ya utambulisho kutoka kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa anakoishi mwombaji.

IV. ZINGATIA

- a) Waombaji wote ambao walishafukuzwa katika kozi za mafunzo ya awali ya uaskari magereza hawaruhusiwi kuomba tena;
- b) Barua itakayowasilishwa kwa njia ya mkono au barua pepe (email) haitafanyiwa kazi;
- c) Mwombaji yoyote atakayewasilisha nyaraka za uongo/kugushi (Forged Documents) atakuwa ametenda kosa la jinai hivyo atachukuliwa hatua kali za kisheria.

Imetolewa na:


Mzee R. Nyamka

KAMISHNA JENERALI WA MAGEREZA